AUSCO

Programu ya Maelekezo ya Kitamaduni nchini Australia

# Ajira

Rahisi Kusoma



Kuwa na kazi itakusaidia kujenga kwa siku za baadaye nchini Australia.



Unapofika labda hutaweza kupata kazi mara moja.




Inaweza kuchukua muda kupata kazi.




Unaweza kukabiliana na changamoto:

- huna uzoefu wowote wa kufanya kazi nchini Australia




- wewe huwezi kuzungumza Kiingereza vizuri sana



- wewe hujui mtu yeyote ambaye anaweza kukusaidia kupata kazi



- ujuzi ulionao sio sahihi kwa kazi nchini Australia




- sifa ulizo nazo hazitambuliwi nchini Australia



Kutulia kwenye nyumba yako mpya inaweza:

- kusababisha hisia za kusisitika
- kuwa changamoto



Kumbuka – inachukua muda.




Hatua za kwanza ambazo wewe unahitaji kujishughulisha nazo ni kama vile:

- kujifunza Kiingereza




- kuchukua kazi ya kwanza inayotolewa



Idara ya Huduma za Binadamu ina huduma za msaada ambazo unaweza kutumia (Department of Human Services - DHS):

- malipo ili kuwasaidia watu ambao hawana kazi au hawana ajira



- msaada kupata kazi



- msaada kupata mafunzo



Serikali ya Australia haitaki watu kutegemea malipo.



Wanataka watu:

- kuendeleza ujuzi wao wa kazi
- kutafuta kazi



Wewe unaweza kupata maelezo zaidi kwenye tovuti ya Idara ya Huduma za Binadamu. www.humanservices.gov.au

## Maadili ya kazi nchini Australia



Kuwa na kazi huko Australia inamaanisha zaidi ya kupata pesa tu.



Watu wa Australia wanaamini kazi ni sehemu muhimu ya nafsi yao –
kuwa nani.



Kuwa na maadili mazuri ya kazi ni muhimu wakati una kazi.




Maadili mazuri ya kazi ina maana:

- unachukua kazi yako kwa makini
- unafanya kazi yako vizuri
- hujisikia vizuri kwa sababu umefanya vizuri



Huenda wewe ukahitaji kuchukua kazi kwenye ngazi ya chini kuliko ngazi yako ya kawaida kufanya kazi.

Si mbaya au kosa.



Inaweza:

- kukupatia pesa ili kusaidia wewe kutunza jamii yako



- kusababisha ukapata kazi bora



Nchini Australia wanaume na wanawake wanafanya kazi.

Wanatendewa sawa katika sehemu ya kazi.

# Kulipia ushuru



Wewe unaweza kupata fedha kupitia:


- kazi yako





- biashara iliyo yako




- Ushuru wa Bidhaa na Huduma (Goods and Services Tax - GST)




- riba kutoka kwa fedha unazo katika akaunti yako ya benki




Serikali ya Australia inachukua baadhi ya pesa unazopata. Inaitwa ushuru au kodi.



Wanatumia ushuru kwenye huduma kama vile:

- ustawi – msaada kwa watu wanaohitaji



- malipo kwa watu ambao hawana ajira



- barabara



- afya




Wewe unahitaji Nambari ya Faili ya Ushuru (Tax File Number - TFN) kutoka Ofisi ya Ushuru wa Australia (Australian Taxation Office - ATO) ikiwa unapanga:



- kupata pesa kutoka kazi yako




- kupata malipo kutoka kwa Serikali



Wewe unaweza kupata maelezo zaidi kuhusu ushuru kwenye tovuti ya ATO.
[www.ato.gov.au](http://www.ato.gov.au)

## Kupata kazi



Kutafuta kazi ni kitu wewe unachohitaji kufanya mwenyewe.



Ni moja ya mambo muhimu unapowasili nchini Australia.



Wewe unaweza kupata msaada ili kutafuta kazi.



Unahitaji kufanyia bidii katika:

- kutafuta kazi
- kupata kazi
- kuitunza kazi yako




Kunazo njia tofauti ambazo wewe unaweza kupata kazi:

- uliza marafiki na jamii yako kama wanajua kuhusu kazi zozote zile




- sikiliza ushauri wa Centrelink i na kufanya kile wanachosema

- kujiandikisha na
  - jobactive
    www.jobs.gov.au/jobactive




au

  - Huduma za Ajira za Ulemavu (Disability Employment Services)
    www.dss.gov.au/our-responsibilities/disability-and-cares/programmes-services/disability-employment-services



- tumia tovuti ya Serikali ya Australia yenye Utafutaji wa Kazi (JobSearch)
  www.jobsearch.gov.au




- angalia
  - magazeti



  - bodi za taarifa za jamii




  - maeneo ya kazi kwenye mtandao



  - vitabu vya simu



- pata msaada kutoka kwa shirika la ajira



- jitolea – kufanya kazi isiyolipwa ambayo inasaidia jamaa



Kujitolea kunaweza kukusaidia:

- kuendeleza ujuzi



- kupata uzoefu wa kikazi



- kukutana na watu ambao wanaweza kukusaidia wewe kupata kazi ya kulipwa



- kufanya shughuli



- kuonyesha watu ambao unaweza kufanya kazi kwa bidii



- kujifunza kuhusu kufanya kazi nchini Australia



Wewe unaweza kupata maelezo zaidi juu ya kujitolea kwenye tovuti ya Kujitolea Australia (Volunteering Australia).
www.volunteeringaustralia.org

# Sifa kutoka nchi za ng'ambo

## Kutafsiri sifa zako kuelekea Kiingereza




Ni muhimu:

- kupanga sifa zako na nyaraka zingine za kikazi zitafsiriwe kuelekea Kiingereza




- kufanya utafiti kama sifa zako zinatambuliwa nchini Australia



Itakuwa rahisi kwa watu ambao wanaweza kukupa wewe kazi kujua nini unachoweza kufanya.

Wewe unaweza kutia maombi mtandaoni ili kupata nyaraka zako kutafsiriwa kwa kutembelea https://translating.dss.gov.au




Nyaraka zako zitafsiriwa kuelekea Kiingereza kisha zitatumwa kwako.




Haitakugharimu pesa zozote.

## Kupata sifa zako kutambulika




Kuwa na sifa zako kutambuliwa kutakupa nafasi nzuri ya kupata kazi kufanya kazi yakawaida kwako.



Baadhi ya ajira itakuwezesha kufanya kozi ili uweze kubadilisha sifa zako ili kufikia viwango vya Australia.

Hizi huitwa kozi za daraja.




Wewe unaweza kupata maelezo zaidi kuhusu jinsi unavyoweza kupata sifa zako kutambuliwa kwenye tovuti ya Idara ya Elimu na Mafunzo (Department of Education and Training).
www.internationaleducation.gov.au


Kumbukumbu za Utambuzi nchini Australia (Trades Recognition Australia - TRA) inaweza kukusaidia wewe ikiwa unafanya kazi katika mojawapo ya viwanda hivi:




- uhandisi



- ujenzi



- kazi ya chuma



- umeme



- upishi




Wanaweza kukupa wewe cheti ambacho kinajulikana nchini kote Australia.



Wewe unaweza kupata maelezo zaidi kwenye tovuti ya TRA.
[www.tradesrecognitionaustralia.gov.au/](www.tradesrecognitionaustralia.gov.au/)

# Kupata Kazi


## Wasifu




Ufupisho wako ni hati kuhusu:

- wewe pamoja na wewe ni nani
- sifa gani ulizonazo
- uzoefu wako – kazi gani uliyofanya kabla

Wewe utaulizwa kupatiana ufupisho wako wakati unapotia maombi ya kazi.




Ufupisho wako uwe:

- kuchapishwa kwenye kompyuta
- kuchunguza makosa yoyote ya herufi



Ikiwa huna ujuzi wa kazi unaweza kuweka vitu vingine katika ufupisho wako ili kuonyesha kuwa utakuwa mzuri kwa kazi:

- kazi ya kujitolea



- kozi za mafunzo au kujifunza



- uzoefu wa maisha uliyokuwa nayo




Huduma kama jobactive zinaweza kukusaidia wewe kuandika ufupisho wako.

Wewe unaweza kupata maelezo zaidi kuhusu jobactive kwenye tovuti ya Idara ya Kazi na Biashara Ndogo (Department of Jobs and Small Business). www.jobs.gov.au/jobactive

## Kwenda kwenye mahojiano



Nchini Australia, kuna watu wengi wanajaribu kupata kazi sawa.



Kabla ya kupata kazi, unaweza kuulizwa kwenda kwenye mahojiano.



Mahojiano ni wakati amabpo wewe unakutana na watu ambao wewe unaweza kuwafanyia kazi pamoja na kuongea nao kuhusu kazi.



Wewe utahitajika kuongea kuhusu:

- elimu yako



- ustadi wako



- uzoefu wako wa kazini



- kwa nini ungependa kuwa mtu mzuri kwa kazi hiyo



Katika tamaduni fulani sio heshima kuzungumza juu yako mwenyewe.



Katika Australia unahitaji kuzungumza juu yako mwenyewe ili uweze kupata kazi.



Katika safari yako ya Australia umeonyesha:

- ujasiri – unaweza kuwa na nguvu wakati vitu si rahisi
- uamuzi – unafanya kazi kwa bidii kufikia malengo yako



Hizi ni sifa nzuri.

Watu ambao wanaweza kukupa kazi wanajua hili pia.

## Wakati wewe unayo kazi



Kuwa na maadili mazuri ya kazi itasaidia kutunza kazi yako.



Kuna mambo mengine ambayo unapaswa kukumbuka wakati una kazi:


- uwahi kufika – usiwe kuchelewa
- ikiwa huwezi kuwahi, waambie watu unaowafanyia kazi haraka iwezekanavyo



Endeleza na kazi wakati unafanya kazi.

Chukua mapumziko wakati unavyoambiwa.





Matatizo madogo ya kibinafsi sio sababu nzuri ya kukosa kwenda kazini.

Kosa kwenda kazini tu, kama ikiwa wewe:

- upo mgonjwa
- unayo hali ya dharura



Uliza maswali ikiwa wewe haujaelewa nini cha kufanya.

Uliza:

- bwana wako
- mfanyakazi mwingine



Watazame wengine ili wewe uweze kujifunza.



Uliza kama unaweza:

- kujaribu kazi mpya
- kuwa na majukumu mapya – mambo unayohitaji kuyafanya




Jenga uhusiano mzuri na watu kazini.

Jaribu kutotumia muda mwingi kuzungumza wakati unapaswa kufanya kazi.

Tenda wengine kwa heshima – jinsi unavyotaka kutendewa.




Utakuwa unafanya kazi na watu ambao wana tofauti:

- utamaduni
- dini
- maoni yao – jinsi wanavyoona dunia



Wanaume na wanawake wanatendewa sawa na mahali pa kazi.




Jenga rekodi nzuri ya kazi – kaa katika kazi ileile kwa miezi 6 kama iwezekanavyo.

Wape watu unaowafanya nao kazi onyo kubwa ikiwa unapanga kuacha kazi yako.



Watendee kwa:

- heshima
- uungwana – tabia mzuri

Watakuwa wapendekeza wako kwa kazi yako inayofuata na kuwaambia watu wengine wewe ni aina gani ya mfanyakazi.




Uambie Centrelink ikiwa unapata kazi. Ni sheria.

Kazi iliyolipwa inaweza kuathiri malipo yoyote unayopata.

Australian Government
Department of Social Services

Inaletwa kwako na Shirika la Uhamiaji la Kimataifa kwa niaba ya Idara ya Huduma za Jamii nchini Australia

IOM • OIM